



Nov. 5, 2021

Familia na wafanyakazi wa RPS 205,

Aksante kwa usaidizi wenu wa kutanguliza afya na usalama wa wanafunzi. Kukerebisha hali ya shule na kurudi katika hali ya kawaida wakati wa janga imekuwa ngumu kwetu sote. Wanafunzi, wafanyakazi na familia wetu wanaendelea kufuata mwongozo kutoka Idara ya Afya ya Kaunti ya Winnebago na Idara ya Afya za Umma za Illinois, na inathaminiwa.

Kwa lengo la kuweka wanafunzi wetu wakiwa na afya njema na kupunguza kukatiza, na kukomesha kuenea kwa COVID-19, tunahitaji wanafunzi wote wa shule ya kati na sekondari wanaoshiriki katika masomo ya ziada au michezo kwa:

1. Kuchukua fursa ya chanjo ya bure ya COVID-19; au
2. Kushiriki katika upimaji wa COVID-19 wa kila wiki kupitia SHIELD Illinois.

Kuanzia Jumatatu, NOV 15. Wanafunzi wote wa shule ya kati na sekondari ambao wanashiriki katika shughuli ya ziada au michezo lazima washiriki katika upimaji wa kila wiki wa COVID-19 katika shule yao ikiwa bado hawajapata chanjo ya COVID-19. Hii ni pamoja na klabu ya riadha, sanaa, na shughuli za kabla na baada ya shule.

KWA NINI SHIELD utoa upimishaji? Wanafunzi katika timu au klabu hutumia muda kwa pamoja nje siku ya kawaida ya shule, na tunataka kuhakikisha kuwa ni salama. Mazoezi, michezo na shughuli sitaingizwa ndani ya jingo kadiri hali ya hewa inavyozidi kuwa baridi. Hiyo pia inamaanisha kuwa hatari ni kubwa zaidi kwa maambukizi, na kuna hatari kubwa tena ya kughairiwa, kuwekwa karantini na kukosa fursa ya mazoezi kwa wanafunzi.

Ugunduzi chanya wa SHIELD Illinois unaweza kutambua COVID-19 kabla ya dalili na mapema kuliko kipimo kingine, ni pamoja na vipimo vya haraka. Hii inamaanisha kwamba mwanafunzi anawezwa kugunduliwa kama yupo na virusi – na kujitenga na wanafunzi wenzako kabla ya kuambukiza na kueneza virusi.

- Jifunze mengi na kujiandikisha kwa chanjo: wchd.org/covid-19
- Jifunze mengi kuhusu na SHIELD Illinois: uillinois.edu/shield
- Ikiwa una maswali, au wasiwasi au maoni, tafadhali ziwasilishwe kwa kutumia Let's Talk: rps205.com/contact-us/lets-talk

Jinsi SHIELD Illinois inatumika: mara moja kila wiki, wanafunzi wataombwa kutema au kudondosha kwenye bomba ndogo ya plastiki. Upimaji unatafuta jeni tatu ya virusi ya SARS-CoV-2, au COVID-19.

Wanafunzi watachukua upimaji wa PCR shuleni badala ya kutembelea ofisi ya daktari, kituo cha huduma ya haraka au duka la dawa. Matokea ya kawaida hupatikana masaa 12-48 baada ya kupimwa.

Tunatarajia kila kupimo kwa mwanafunzi kuchukua dakika chache tu, na inatolewa katika kila shule ya kati na sekondari:

Jumatatu: Auburn

Jumanne: East, Lincoln, RESA

Jumatano: Guilford, Jefferson, Marshall MS

Alhamisi: Barbour, Kennedy, Roosevelt

Ijumaa: Eisenhower, Flinn, West